JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P. 38
GEITA
Simu: 028-2520004
Nukushi: (028) 2520040
Baruapepe: rbcgeita@pccb.go.tz
Website: www.pccb.go.tz

GEITA – OKTOBA 09, 2020.

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

TAKUKURU MKOA WA GEITA YATEMESHA MAFISADI JUMLA YA SHILINGI 191,198,624.92

NDUGU WANAHABARI
Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia kibali cha kukutana siku ya leo. Aidha ninawashukuru ninyi wote kwa kuitikia wito kuja kushiriki mkutano huu kwa ajili ya kuuhabarisha umma juu ya kazi ambazo zimetekelezwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba, 2020. Karibuni sana ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Geita.

NDUGU WANAHABARI
Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2020 tumeweza kutekeleza majukumu ya Uchunguzi na Mashtaka, Uelimishaji umma juu ya Mapambano dhidi ya Rushwa, Uzuiaji Rushwa pamoja na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

NDUGU WANAHABARI
Uchunguzi na Mashtaka wa tuhuma za Rushwa umewezesha uokoaji wa fedha jumla ya shilingi **191,198,624.92** zilizofanyiwa ubadhirifu kwa njia mbalimbali za Rushwa na dhuluma.

- Kiasi taslimu cha shilingi **30,124,323/=** ni fedha zilizorejeshwa kutokana na uchunguzi katika vyama vya ushirika kwa mchanganuo ufuatao;
    - Shilingi **13,194,323/=** zimetokana na uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu katika chama cha kuweka na kukopa cha Geita SACCOS, Shilingi **16,630,000** za chama cha Ushirika wachimbaji wadogo wadogo cha Ikuzi wilayani Bukombe na Shilingi **300,000/=** zimetokana na uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu katika chama cha kuweka na kukopa cha Katoma SACCOS.

- Kiasi cha shilingi **1,527,000/=** ni fedha zilizookolewa kutokana na mishahara hewa katika sekta ya Elimu ambazo zimerejeshwa serikalini.

- Kiasi cha shilingi **1,309,600/=** ni posho za waandishi wa habari wanachama wa chama cha waandishi wa habari Mkoani Geita (GPC) ambazo zilikuwa zimefanyiwa ubadhirifu ambazo tayari chama kimekabidhiwa.

- Kiasi cha shilingi **25,992,000/=** ni fedha walizorejeshewa wananchi kutokana na dhuluma, hongo, michango na fedha mbalimbali walizotozwa kinyume na taratibu na sheria za nchi na fedha hizo zimekabidhiwa kwa wanyonge hao. Miongoni mwa fedha hizo, shilingi 5,500,000/= ni fedha ambazo mwalimu mstaafu aitwaye ADELA ANDREA FAUSTINE alikuwa amedhulumiwa na mkopeshaji ISACK MASWI NYAMHANGA Wilayani Chato kwa njia za Mikopo umiza ambazo mstaafu huyo amekabidhiwa leo. Mkopeshaji anachunguzwa na Takukuru kwa kujihusisha na vitendo vya kijinai na dhuluma katika kuendesha biashara hiyo kwa riba kubwa. Na wahanga wakubwa wa mikopo hiyo ni watumishi wa umma na wastaafu. Mfano mstaafu ADELA ANDREA FAUSTINE alikopa Shilingi 700,000/- na baada ya kulipwa pensheni, kwa njia za vitisho alilazimishwa kurejesha Shilingi 7,000,000/- ambayo ni sawa na riba ya asilimia 900%. Pia mtuhumiwa alipofanyiwa upekuzi alikutwa na kadi za benki 64 ambazo ni za wakopaji ambao ni watumishi wa umma.

- Shilingi **2,601,000/=** ni fedha zilizookolewa kutokana na malipo na manunuzi hewa katika sekta ya Elimu na TAMISEMI

- Shilingi **4,044,000/=** ni fedha za malipo ya deni la wakulima wa pamba ambazo zielipwa kwa wakulima waliodhulumiwa na wahasibu wa AMCOS za Nyamigogo (shilingi 2,611,000/= na Nyamalimbe shilingi 1,433,800/=).

- Shilingi **69,690,000/=** ni fedha zilizotokana na biashara haramu ya Mkaa uliokamatwa na maafisa TAKUKURU wilayani Bukombe kisha mkaa huo kupigwa mnada na fedha hizo kulipwa serikalini kupitia akaunti ya wakala wa misitu TFS.

- Shilingi **7,943,400** ni malipo ya fidia kwa wananchi kwa ajili ya Mashamba na Mazao eneo la Nyankumbu kutokana na Ujenzi wa barabara ya lami ya Geita- Bwanga- Biharamulo mwaka 2005/2008. Wananchi hao wamelipwa fedha hizo na taratibu zilizobaki ni kuhakikisha shimo linafukiwa kwa usalama wa wananchi ili eneo hilo liweze kutumika kwa shughuli za kiserikali.

- Jumla ya Kiasi cha shilingi **47,967,301.92** kimeweza kulipwa zikiwa ni kodi zilizokwepwa na ushirika wa Nyamatagata katika biashara wanayofanya ya kuuza vyuma chakavu kutoka mgodi wa dhahabu wa Geita (GGML) ambapo TRA **(Sh. 45,577,153.45)** na Halmashauri ya Mji Geita **(Service Levy Sh. 2,390,148.47)**.

- Aidha katika kipindi hiki tumeweza kusaidia kurejesha kiwanja Namba **03 Kitalu 'C'** kilichopo mtaa wa Mwatulole kwa mama aitwaye DOTTO JOHN aliyekuwa amedhulumiwa na mfanyabiashara akishirikiana na watumishi wasio waaaminifu wa Idara ya Ardhi kwa lengo la kujenga kituo cha mafuta.

Katika kipindi hiki cha Julai hadi Septemba, 2020 pamoja na fedha zilizotemeshwa mikononi mwa mafisadi hawa, Taasisi imeweza kufungua mashauri matatu (03) mahakamani ambapo jumla ya washtakiwa 07 wakiwemo watumishi wa umma 02 na watu binafsi 05 wanaendelea kujibu mashtaka yao. Jumla ya mashauri yaliyoendeshwa mahakamani ni 41 ambapo 6 yalitolewa maamuzi na Jamhuri kushinda.

Aidha katika kipindi husika jumla ya malalamiko dhidi ya rushwa na makosa mengine 113 yamepokelewa na kinara wa kulalamikiwa ni sekta ya Serikali za Mitaa malalamiko 36, Madini 13, Afya 09, Ardhi 08, Fedha 07, Mahakama 06, Ushirika 05, Elimu 05, Biashara 04, Polisi 04, Siasa 04, Sekta binafsi 03, Misitu 02, Kilimo 02, Dini 01, Nishati 01, Usafirishaji 01, Huduma za jamii 01 na Ujenzi 01.

Uchunguzi wa awali wa malalamiko haya umefanyika ambapo jumla ya majalada ya uchunguzi 06 yamefunguliwa, taarifa 01 imehamishiwa ofisi nyingine, taarifa 21 zilitolewa ushauri na hatua za kiutawala na taarifa 85 zinaendelea kufanyiwa kazi. Katika kipindi hicho jumla ya majalada 06 uchunguzi wake umekamilika.

NDUGU WANAHABARI

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2020 TAKUKURU imetekeleza jukumu la ***kuhamasisha umma kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa*** kwani bila ushiriki wa dhati wa jamii nzima mapambano haya hayataleta tija iliyokusudiwa.

Tumeendelea kutumia mbinu mbalimbali za kuelimisha kupitia semina 69, mikutano ya hadhara 84 ikiwa ni sehemu ya kuelimisha wananchi kuchagua viongozi bora na sheria za uchaguzi na makatazo katika kipindi cha kampeni na uchaguzi mkuu 2020 pamoja na elimu ya kampeni ya UTATU, VUNJA UKIMYA KATAA RUSHWA YA NGONO na matumizi ya TAKUKURU APP, ufunguaji wa klabu za wapinga Rushwa 26 na uimarishaji wa klabu za wapinga Rushwa 153 katika Shule za Msingi na Sekondari, vipindi vya Redio 07, taarifa kwa vyombo vya habari 03, maonesho 03, uandishi wa makala 07, mkutano na waandishi wa habari 02 na kugawa machapisho mbalimbali kwa wananchi.

NDUGU WANAHABARI

Kama nilivyoeleza awali kuwa majukumu mengine yaliyotekelezwa ni ***Uzuiaji Rushwa na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa miradi ya maendeleo***. Katika uzuiaji rushwa lengo kubwa ni kufanya uchambuzi wa mifumo ya utendaji kazi ili kuziba mianya ya Rushwa kupitia warsha na matekelezo.

Katika kipindi hiki tumefanya uchambuzi wa mifumo katika Halmashauri Tano za Mkoa wa Geita katika sekta ya fedha eneo la ukusanyaji wa kodi ya Huduma (Service Levy).

Kupitia chambuzi hizo tulibaini yafuatayo:

- Wafanyabiashara wengi hawajui uwepo wa Kodi ya Huduma na wanatakiwa kumlipa nani.
- Halmashauri zote 5 hukusanya kodi ya Huduma kwa wafanyabiashara wenye leseni chini ya asilimia 10% ya leseni zote walizotoa.
- Halmashauri kukosa sheria ndogo ndogo kwa baadhi ya biashara hivyo kushindwa kutoza kodi ya huduma.
- Halmashauri kushindwa kufuatilia madeni mbalimbali kutoka kwa wafanyabiashara hasa ya kodi ya huduma.
- Halmashauri kuwa na vitendea kazi vichache yaani magari pamoja na wahasibu na wahasibu wasaidizi kunakwamisha kuweza kurahisisha ukusanyaji wa kodi ya huduma.

Kufuatia mapungufu haya ofisi imechukua jukumu la kuandaa warsha itakayofanyika kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka 2020 ili kuweza kuweka mikakati ya pamoja na halmashauri, wafanyabiashara, TRA na wadau mbalimbali ili kuwa na uelewa wa pamoja juu ya kodi ya huduma na kurahisisha na kuboresha zoezi la ukusanyaji wa kodi hii.

Aidha miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi **7,184,575,943.02 (**Bilioni Saba, Mia Themanini na Nne Milioni, Mia Tano Sabini na Tano Elfu, Mia Tisa Arobaini na Tatu na Senti Mbili Tu**)** imefuatiliwa katika sekta za Elimu, Maji, na Ujenzi lengo likiwa ni kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa kuzingatia thamani ya fedha (value for money).

Miradi iliyofuatiliwa ni; Mradi wa Usambazaji Maji kwenye Vijiji vya Kabanga Nhomolwa (Mbogwe), na Ujenzi wa Matundu 19 ya choo katika Shule ya msingi Ilolangulu wilayani Mbogwe, Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilometa moja barabara ya CCM – Buseresere (Katoro Geita) , Mradi wa Usambazaji Maji Katika Kijiji cha Lwamgasa Wilayani Geita, Ujenzi wa Mradi wa Maji Katika Kijiji cha Buntizya (Bukombe), Ujenzi wa Matundu 24 ya choo katika shule ya Msingi Bomani wilayani Bukombe , Mradi wa Maji Mnekezi (Chato) na Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji Chato Mjini.

Ufuatiliaji huo ulibaini changamoto ya miradi kuchelewa kukamilika kwa wakati na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi. Jitihada zimefanyika kuwezesha marekebisho ya kasoro hizo kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na Taasisi kutoa Elimu kwa wadau kuhusu manunuzi ya umma na usimamizi wa miradi pia kuzingatia taratibu na miongozo inayotolewa na watoa fedha.

NDUGU WANAHABARI

KUELEKEA UCHAGUZI MKUU 2020.

Sote tunafahamu kuwa mwaka huu mwezi Oktoba, 2020 tutakuwa na Uchaguzi Mkuu. Uchaguzi huu unapaswa kuendeshwa na kusimamiwa kwa uadilifu na umakini mkubwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili haki, usawa, uhuru na demokrasia viweze kustawi, kuendelezwa na kudumishwa.

Ni vyema watanzania wakatambua kuwa uchaguzi ni fursa ambayo wanaitumia kutafakari mustakabali wa maendeleo ya maeneo yao na Taifa, ni fursa kuainisha changamoto zote zinazowakabili kama jamii kwenye maeneo yao kama vile barabara ,maji, zahanati na ni fursa ya kutathimini uwezo wa viongozi waliochaguliwa katika uchaguzi uliopita endapo walikuwa na mchango wowote katika kuwaletea maendeleo waliyotarajia.

Pia watanzania watambue kuwa lengo la uchaguzi ni kupata kiongozi mwadilifu, mwaminifu, uzoefu wa eneo la uchaguzi analogombea, awe na dira ya kuongoza, mchukia rushwa kwa maneno na vitendo na anayezingatia utii wa sheria, kanuni na taratibu za nchi. Vile vile watambue thamani ya kura kuwa ni MAENDELEO, AMANI, UTULIVU na HAKI.

Aidha wananchi watambue kuwa wananchi wapokea na watoaji Rushwa hawawezi kuhoji masuala mbalimbali ya maendeleo kwa viongozi wao. Kwa kuzingatia umuhimu wa uchaguzi huo, TAKUKURU tumejizatiti kufuatilia kwa umakini hatua kwa hatua uchaguzi huu na wale watakaojihusisha na vitendo vya rushwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

NDUGU WANAHABARI

Jukumu la kupambana na Rushwa ni letu sote mkiwemo ninyi. Mnaombwa kusaidia kufichua wagombea watoa rushwa kwa kutoa taarifa TAKUKURU kwani mapambano dhidi ya rushwa ni jukumu letu sote. Vyombo vya habari ninaomba mtumie fursa mliyo nayo ya kuifikia jamii kwa kuwaelimisha kupitia vyombo vyenu kutambua thamani na umuhimu wa kura zao katika kupata viongozi walio bora.

MWISHO

Mikakati ya TAKUKURU Mkoa wa Geita kwa kipindi cha Oktoba – Desemba, 2020 ni kuendelea kutatua kero za wananchi zinazohusiana na vitendo vya Rushwa na dhuluma za aina mbalimbali, kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wananchi ili waelewe haki na wajibu wao katika kuchagua viongozi bora katika uchaguzi mkuu 2020, kupata huduma na kuendelea kuwaelimisha watumishi wa sekta za Umma na binafsi kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha ni wito wa TAKUKURU mkoa wa Geita kwa watumishi wa umma mkoani humu kuzingatia kanuni na taratibu pindi wanapohitaji huduma za mikopo ili kuepukana na mikopo umiza kama nilivyoeleza hapo juu. Na wakopeshaji ni vyema wakazingatia kanuni za biashara ya ukopeshaji fedha maana kinyume na hivyo watakuwa wanatenda makosa ya jinai na wataendelea kuchukuliwa hatua za kisheria.

Wito wetu kwa wananchi wa mkoa wa Geita, waendelee kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa, kuwa waadilifu kwa kutojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa, washiriki pia kutoa taarifa za vitendo vya rushwa TAKUKURU kwa kupiga simu ya bure 113, *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au kupitia TAKUKURU APP.

Sote Tuseme *"KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU"*

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

IMETOLEWA NA:
Leonidas R. Felix
MKUU WA TAKUKURU (M) GEITA